# Waziri ataka wavuvi kuchangamkia fursa



Na Anastazia Anyimike

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega amewataka wadau wa mifugo na uvuvi kuchangamkia fursa zitakazotokana na Jukwaa la Mifumo ya Chakula Afrika (AGRF 2023) ambao marais wa nchi 15 za Afrika wametumiwa mwaliko.

Ulega alitoa rai hiyo wakati wa kikao cha maandalizi ya jukwaa hilo litakalofanyika Septemba 5 hadi 8, mkoani Dar es Salaam kilichoenda sambamba na kusajili wadau wa mifugo na uvuvi kushiriki kwenye kongamano hilo.

Alisema kwa mara ya kwanza mifugo na uvuvi inakuwa ni sehemu ya kongamano la mifumo ya chakula Afrika na kubainisha dhamira ya serikali katika kutekeleza dhana ya mabadiliko na kuchangia katika kutatua matatizo ya mifumo ya chakula Afrika.

Ulega alisema wizara ina uwezo wa kuchangia katika mabadiliko ya mfumo mzima wa chakula na kwa kushirikiana na wadau wa sekta binafsi wamedhamiria kuwa watatuzi wa matatizo yanayokabiliwa na mfumo mzima wa chakula.

Alisema Wizara ya Mifugo na Uvuvi imeweka mikakati mikubwa katika kuongeza mchango wake kwa pato la taifa kutoka asilimia 6.7 mwaka 2022/23 hadi kufikia kwa asilimia 10 kwa mifugo na kutoka asilimia 1.8 hadi asilimia tatu kwa uvuvi.

Naye Mwenyekiti wa Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF), Angelina Ngalula alisema ili kupata manufaa ya kongamano hilo lazima Watanzania watafute thamani ya Tanzania, kuwa na mpango mkakati wenye tija na kuwa na takwimu halisi na zenye ushahidi.

Akitoa salamu za wadau wa mifugo, Hamoud Salim aliahidi kuwa wadau wa sekta ya mifugo wanashiriki na kutumia ipasavyo fursa zitokanazo na kongamano na Watanzania kupewa kipaumbele hususani katika maonesho.

CamScanner

Fedha hizo zilitolewa na

vinywaji, Chalami
fedha hizo zitumi

HABARI LEO UK 15.

# Ng'ombe 800 wakamatwa kwa kuharibu mashamba

**Na Muhidin Amri, Tunduru**

MKUU wa Wilaya ya Tunduru, Julius Mtatiro amesema wamekamata zaidi ya ng'ombe 800 waliokutwa wakila katika mashamba na kuharibu mazao ya wakulima katika maeneo mbalimbali wilayani humo.

Alisema ng'ombe hao wamekamatwa kutokana na doria na oparesheni kubwa inayoendelea ya kuwaondoa wafugaji wote wanaofanya ufugaji na kuingiza mifugo kwenye maeneo yasiyoruhusiwa kisheria.

Mtatiro alisema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake na kusisitiza kuwa ni lazima wafugaji wote kwenda katika vitalu vilivyotengwa kwa ajili ya kufugia badala ya kuendelea na ufugaji holela.

"Kuna tabia ya baadhi ya wafugaji kupeleka kwa makusudi mifugo yao kwenye mashamba na kuharibu mazao ya wakulima jambo linalosababisha migogoro mikubwa kati ya wakulima na wafugaji hao," alisema.

Alisema mwaka 2019 serikali wilayani Tunduru ilitenga vitalu 250 ili vitumike kwa ajili ya ufugaji. Hata hivyo, ni vitalu 125 tu vimelipiwa na kutumika kwa ajili ya kazi hiyo.

CamScanner